



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NASERIKLI ZA MTA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. GDC/I.20/9/66

14/05/2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepokea kibali cha Ajira chenye Kumb. Na.FA.228/613/01/B/081 cha tarehe **22 Aprili, 2024** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mbadala, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita anatangaza nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa watazania wenye sifa za kujaza nafasi kama zilivyoorodheshwa katika Tangazo hili.

1.0 MTENDAJI WA KIJJI DARAJA LA III (NAFASI 8)

1.1 Sifa za muombaji

- i. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
- ii. Awe na Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Rasilimali watu, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha au Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2. Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezai wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Kuratibu Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.

- vii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Kijiji.
- ix. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.3 Mshahara

- i. Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani **TGS B** kwa mwezi.

1.4 MASHARTI KWA UJUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini.
- ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma.**
- iii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika Kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wenye kuaminika.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha nne, Kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- vii. "Testimonials, Provisional Results, Statement of Result" na hati za matokeo kidato cha Nne na Sita (form IV na VI Result Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
- viii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU).
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. Waombaji kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia Maelezo yaliyo katika Waraka Na. **CAC.45/257/01/D/140** wa Tarehe **30 Novemba, 2010.**

- xii. Uwasilishwaji wa taarifa za sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua Stahiki za Kisheria.
- xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **27/05/2024**.
- xiv. **MUHIMU:** kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Aidha, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,
S.L.P 139,
GEITA.**

- xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa ajira(Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo <https://portal.ajira.go.tz/> Anuani hii pia inapaikana kwenye Tovuti ya Sekretariat ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa Recruitment Portal”).
- xvi. Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulio ainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

Karia R. Magaro
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**